

Msigano wa Majina ya ‘Walemvu’ katika Jamii ya Wazungumzaji Kiswahili: Mifano kutoka Tanzania

Elizabeth G. Mahenge

Ikisiri

Walemvu wamekuwa wakilalamikia matumizi ya majina yanayowarejelea katika jamii ya wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili. Jambo hili nililigundua wakati nilipokuwa ninafuatilia vipindi vyta walemvu katika runinga na radio nchini Tanzania. Majina kama vile kilema, kiwete, kipofu, zeruzeru, asiyesikia na mengineyo ni baadhi ya majina ambayo wazungumzaji wamekuwa wakiyatuma kwa muda mrefu (yaani tangu zamani za kale) lakini kwa upande mwagine wanaoitwa majina hayo wamekuwa wakiyatataa. Makala haya yanachunguza msigano wa majina wanayoitwa ‘walemvu’ nchini Tanzania. Vilevile, makala yatazungumzia vikwazo mbalimbali wanavyokutana navyo walemvu katika mawasiliano. Mambo haya yana umuhimu mkubwa wa kuzungumziwa katika makala haya kwani lengo kuu la kuwepo kwa ‘lugha’ katika jamii ni mawasiliano. Pia makala haya yatatoa mapendekezo mbalimbali kuhusiana na mambo ambayo yameshughulikiwa katika utafiti huu.

1.0 Utangulizi

Ulemavu ni hali ya kupoteza kiungo au kuwa na kikwazo cha kushindwa kujishughulisha na maisha ya kawaida sawia na watu wengine (ILO, 2007). Kikwazo hicho kinaweza kuwa ni kutokana na hali ya mwili, akili au sababu za kijamii ambazo kwa pamoja zinasababisha kushindwa kujumuika na wengine. Makala haya yamelenga kuchunguza msigano wa majina yanayotumika kuwaita walemvu katika jamii ya Watanzania. Katika kulifikia lengo hili tutapitia maana ya ulemavu, historia ya walemvu nchini Tanzania na maana ya lugha. Kwa kuwa lengo kuu la lugha ni mawasiliano makala haya pia yataongelea vikwazo vinavyojiteza katika kufanya mawasiliano na watu wenye ulemavu.

Utafiti huu ulifanyika katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambako mwandishi wa kazi hii alikuwa akisoma darasa moja na baadhi ya walemvu waliofafitiwa. Sampuli ya utafiti huu ilijumuisha walemvu wa ngozi wawili (2), walemvu wa viungo watatu (3) na wasioona kumi (10). Jumla ya wahojiva walikuwa kumi na tano (15). Wanawake walikuwa wanane (8) na wanaume walikuwa saba (7). Umri wao ni kati ya miaka 20 hadi 35. Wanafunzi hawa walikuwa wakisoma shahada mbalimbali kama vile Elimu, Sosholojia na Sheria mnamo mwaka 2002-2006.

2.0 Maana ya Ulemavu

Kwa mujibu wa asasi, wataalamu na jamii kwa ujumla inaonekana kuwa kumekuwapo na tofauti ya maana katika istilahi ‘ulemvu’. Miogoni mwa fasili hizo ni ile inayosema kwamba ulemavu ni hali ya kupoteza kiungo au kuwa na

kikwazo cha kushindwa kujishughulisha na maisha ya kawaida sawia na watu wengine (ILO, 2007). Pia inafafanuliwa kuwa ulemavu ni kupoteza au kuwa na kikwazo cha kushindwa kupata fursa katika jamii sawasawa na watu wengine kutokana na hali ya kimaumbile, kiakili au sababu za kijamii (*United Republic of Tanzania*, 2010:2). Vivyo hivyo, inaelezwa kuwa ulemavu ni hali ya kupoteza au kuwa na kikwazo cha kushindwa kujishughulisha na maisha ya kawaida sawia na watu wengine kutokana na hali ya mwili, akili, au sababu za kijamii (Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, 2004). Swali la kuijiliza hapa ni je, ulemavu ni hali ya kupoteza? Kupoteza nini?

Ukiachilia mbali fasili za ulemavu kwa mujibu wa asasi hizi chache, hatuna budi pia kupitia fasili ya dhana hii kwa mujibu wa watu wenye ulemavu wenyewe. Mathalani, Rutachwamagyo (2008:23) anaelezea kuwa "ule mavu ni hali ya jamii kutotoa fursa au haki kwa mtu aliye na kilema ili ajumuike katika shughuli za kijamii kwa usawa." Vilevile, inafafanuliwa kuwa kwa kawaida "ule mavu huwa ni wa fikra na mielekeo hasi; si wa maumbile" (Apalei, 2010:76). Kwa mujibu wa Apalei (keshatajwa), mtu ambaye hana kasoro za kimaumbile anaweza kuwa mlemavu kutokana na mitazamo hasi walijonayo wanajamii na mtu mwenye kasoro za kimaumbile akawa si mlemavu. Kamusi pia ni chanzo muhimu cha fasili ya maneno mbalimbali, kwa mfano Kamusi ya Kiswahili Sanifu inamwelezea mlemavu kuwa ni "mtu aliye na kiungo cha mwili chenye hitilafu"; "ni hali ya kulemaa" (TUKI 2000:433). Kutokana na fasili hizi, makala haya yanaona kuwa tunapozungumzia watu wenye mahitaji maalumu au wale mavu (kama ambavyo majina haya mawili yatatumika kuwarejelea) ni pamoja na wasioona, viziwi, bubu, bubuviziwi, bubuviziwiwasioona, wale mavu wa viungo na albino.

3.0 Historia ya Wale mavu Nchini Tanzania

Tangu mwaka 1961, serikali kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii imekuwa ikitoa huduma kwa watu wenye ulemavu bila kuwa na sera. Sera ya Taifa ya Watu Wenye Ulemavu ijulikanayo kama *National Policy on Disability* imetungwa mwaka 2004. Vilevile, Tamko la Haki za Watu wenye Ulemavu linalojulikana kama *UN Declarations of Human Rights for People With Disabilities* limetolewa mwaka 1975. Pia Tanzania iliridhia makubaliano kuhusu fursa na haki sawa kwa watu wenye ulemavu ambao unajulikana kama *Standard Rules of the Equalization of Opportunities for Persons with Disability* mwaka 1993 (URT, 2004).

Kwa muktadha wa Bara la Afrika, Tanzania ni mwanachama na imesaini mkataba wa malengo ya utekelezaji wa haki za watu wenye ulemavu ambao unajulikana kama *Plan of Action for the African decade of Persons with*

Disabilities mwaka 1999 – 2009. Pia Tanzania ni mwanachama wa taasisi ya Kiafrika inayojishughulisha na kuwawezesha walemaru kuishi baada ya kupata ajali. Tanzania ilijiunga na taasisi hii ya *African Rehabilitation Institute* mwaka 1985 (URT, 2004). Mwaka 2001 Tanzania iliingia mapatano ya kimataifa kuhusu ulinzi na uendelezaji wa haki na utu wa watu wenye ulemavu yanayoju likana kama *Comprehensive and Integral International Convention on Protection and Promotion of Rights and Dignity of Person with Disabilities* (URT, 2004). Kwa kipindi chote hicho, serikali imekuwa ikiwahudumia walemaru kupitia sera, miongozo, mapatano na mikataba. Mwaka 2010 ndipo sheria ya watu wenye ulemavu iitwayo *Persons with Disability Act* ilipopitishwa rasmi (URT, 2010). Kwa hiyo, sasa hivi kuna nguvu ya kisheria katika kudai haki za walemaru.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu Zanzibar, na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kwa kushirikiana na Vyuo Vikuu Tanzania, mwaka 2008 waliendesha sensa ya watu wenye ulemavu na kubaini kuwa ni asilimia 8% ya Watanzania wana ulemavu (Mwakyusa, 2008). Vilevile, Shirika la Afya Duniani linakadiria kuwa katika kila jumuiya, asilimia 10% ya watu wake wana aina fulani ya ulemavu wa kimwili na kiakili (Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, h.t:3). Takwimu hizi zinaweza kuongezeka kwa kuwa kuna walemaru wanaofichwa majumbani na hivyo kutokuhesabiwa (Mahenge, 2011). Kutokana na utafiti huo wa Wizara ya Afya na wadau wake, ilibainika kuwa, viwango vya ulemavu ni vikubwa vijijini kuliko mijini. Pia kiwango cha ulemavu ni kikubwa Tanzania Bara kuliko Tanzania Visiwani. Hali hii ni kutokana na kwamba Tanzania bara ni kubwa kijiografia na ina idadi kubwa ya watu ukilinganisha na Tanzania Visiwani. Ulemavu wa macho unaonekana kuongoza kwa idadi kubwa ukifuatiwa na matatizo ya kutembea, uziwi na kadhalika (URT, 2004: iii). Kwa hiyo, idadi ya watu wenye ulemavu nchini Tanzania ni kubwa na hivyo kundi hili linahitaji kufanyiwa tafiti mbalimbali. Mojawapo ya tafiti hizo ni huu wa kuchunguza namna lugha ya Kiswahili inavyowarejelea watu hawa kwa kuwa wamekuwa wakilalamikia matumizi ya lugha hii. Je lugha ni nini?

4.0 Fasili ya Luga

Kwa mujibu wa Besha, "Lugha inachukuliwa kama "tabia" ya kawaida ya mwanadamu, na kwa sababu ya ukawaida huo, si mara nydingi wanadamu wakakaa na kujiuliza kitu hiki (lugha) kikoje" (Besha, 2007:1). Nao Massamba na wenzake (1999:1) wanaelezea kuwa, "Wataalamu wengi wa isimu na lugha wanaelekeea kukubaliana kwamba lugha ni mfumo wa sauti nasibu ambazo hutumiwa na jamii kwa madhumuni ya mawasiliano kati yao." Si hivyo tu, bali Kamusi ya Kiswahili Sanifu nayo inafasili kuwa, "Lugha ni mpangilio wa sauti na maneno unaoleta maana na ambao hutumiwa na watu ili kuwasiliana" (TUKI,

2000: 211). Ukiziangalia fasili hizi za lugha utaona kuwa zinabagua lugha ya alama ambayo ni njia ya mawasiliano kwa baadhi ya walemaru kama vile viziwi, bubuviziwi, na bubuviziwiwasioona.

Kuhusiana na lugha ya alama, Muzale (2004: i) anaeleza kuwa lugha hii ilichipuka nchini Tanzania baada ya viziwi kuanza kukaa pamoja na kulazimika kuwasiliana, hasa katika shule maalumu za viziwi. Lugha ya alama ni mionganoni mwa lugha inayotumiwa na watu wenye ulemaruu kama vile viziwi, bubuviziwi, na bubuviziwiwasioona. Kwa hiyo, kuna haja ya kujumuisha kwenye orodha ya lugha na kutambuliwa rasmi nchini Tanzania. Hivyo, kwa maana pana, tunaweza kusema kuwa, lugha ni njia inayowezesha watu wa kundi fulani kuwasiliana ama kwa maandishi, sauti, alama, ishara, na lugha ya alama mguso. Kama lugha ni njia ya mawasiliano mionganoni mwa wanajamii, je ni kwa kiasi gani lugha hiyo inatumika kuwarejelea walemaru? Katika sehemu ya 6.0 tutawasilisha majina ya walemaru kama wanavyoitwa katika jamii ya wazungumzaji wa Kiswahili nchini Tanzania na pia tutaonesha majina ambayo yanapendekezwa na walemaru wenyewe. Kabla hatujafika kwenye kiini cha makala yetu hatuna budi kueleza japo kwa ufupi vikwazo wanavyokutana navyo watu wenye ulemaruu. Kwa kufanya hivi itatusaidia kupata mwanga kuhusu walemaru na suala zima la mawasiliano katika jamii.

5.0 Vikwazo Wanavyokutana navyo Walemaru katika Mawasiliano

Watu wenye ulemaruu wanakabiliwa na vikwazo mbalimbali kutokana na changamoto kadha za miili yao. Kwa mfano, mlemauu ambaye ni bubukiziwasiyeona anakabiliwa na vikwazo vingi kwa pamoja. Kwanza, ni bubu hivyo anashindwa kuzungumza. Pili, ni kiziwi hivyo anashindwa kusikia sauti, na tatu haoni kwa hiyo anashindwa kuona. Mlemauu huyu anahitaji lugha ya alama ya kupapasa pamoja na maandishi ya nukta nundu ili aweze kuwasiliana na wanaoona au na watu wenye hali kama ya kwake. Kwa upande mwingine, mlemauu wa viungo ambaye hana miguu hushindwa kupanda ngazi katika majengo. Mlemauu huyu anahitaji njia isiyo na ngazi au lifti ili aweze kufika ghorofani (labda ni ofisini, hospitalini au shulenii) ili kuwasiliana na wanajamii wenzake au kupata huduma mbalimbali.

Mlemauu wa macho – aina hii ya ulemaruu inategemea kama ni asiyeona kabisa au anayeona kidogo (mwenye uoni hafifu). Mlemauu asiyeona kabisa anakabiliwa na kikwazo cha kukosekana kwa maandishi ya breili na mashine zake. Kikwazo hiki kinamfanya ashindwe kusoma maandishi yasiyo na nundu kwa kuwa, ili aweze kuwasiliana anahitaji maandishi ya aina hiyo. Mlemauu wa macho ambaye anaona kidogo (mwenye uoni hafifu), anahitaji maandishi yaliyokuzwa kidogo. Mathalani, watu wenye ulemaruu wa ngozi wanakabiliwa na

tatizo hili. Hawaoni maandishi ya ‘kawaida’ kama vile fonti 12 au chini ya hapo na badala yake wanahitaji maandishi yanayotumia fonti kubwa zaidi. Mlemau ambaye ni bubu ana mahitaji tofauti na mlemau ambaye ni bubukiziwi. Bubu ana uwezo wa kusikia kinachozungumzwa ila hawezi kuzungumza. Kwa hiyo, huyu anaweza kuwasiliana kwa vitendo na maandishi na kwa kutoa sauti fulani inayoashiria kuzungumza. Lakini kwa mlemau ambaye ni bubukiziwi – yeze anahitaji lugha ya alama ili aweze kuwasiliana. Kwa hiyo, mlemau huyu anakabiliwa na kikwazo cha kukosekana vitabu vilivyo katika lugha ya alama pamoja na wakalimani wa lugha ya alama, kitu ambacho kinamfanya ashindwe kuwasiliana kwa njia ya kusikia sauti. Kwa hiyo, vyote hivyo kwa pamoja ni vikwazo kwa mlemau katika suala la mawasiliano na/au ujifunzaji. Kila mlemau ana changamoto zake ambazo ni tofauti na za mwingine.

6.0 Msigano wa Majina ya Walemaru katika Jamii ya Watanzania

Kama tulivyokwisha sema toka awali, kwamba kumekuwapo na msigano wa majina wanayoitwa watu wenyewe ulemavu katika jamii ya Watanzania, majina hayo kwa mujibu wa maelezo yao, yanaonekana kuwadhalilisha. Majina haya ni kama vile ‘*kiwete*’, ‘*kilema*’, ‘*kipofu*’, ‘*zeruzeru*’ na ‘*taahira*’ kama tulivyoyataja mwanzoni mwa makala haya. Majina haya yanasaababisha watu wenyewe ulemavu wajisikie vibaya (kufedheheshwa).

Kutokana na hali hiyo, tulilazimika kufanya utafiti huu mdogo. Utafiti huu unatokana na kutoridhishwa kwa walemaru na majina yanayotumika kuwarejelea. Majina hayo yanaakisi ulemavu wao kama ni wa viungo, macho, akili na masikio. Hata hivyo, utafiti wetu umegundua kuwa walemaru wenyewe tatizo la uziwi hawana malalamiko kuhusiana na kuitwa ‘*kiziwi*’ au *viziwi*.’ Wao hawajisikii kudhalilishwa wanapoitwa hivyo (taarifa hii ni kwa mujibu wa mazungumzo ya mtafiti na mwalimu Malise wa Shule ya Uhuru Mchanganyiko, 2010, yaliyofanyika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika semina ya Luga ya Alama ya Tanzania - LOT).

Kuwapo kwa msigano kati ya majina wanayoitwa walemaru ni suala lililokuwapo kwa muda sasa katika jamii ya wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili. Kuwaita majina hayo ambayo hawayataki hakutokani na makusudi au kukosekana kwa majina mwafaka, la hasha! Bali ni kutokana na mazoea ambayo jamii imeijenjea ya kuwaita kwa namna hiyo. Yaani kuwaita kwa kurejelea hali ya viungo vyao au maumbile yao. Utafiti wetu umegundua kuwa kuelimika miongoni mwa walemaru kumewasaidia kuchunguza majina yao haya na kuyaona kuwa yanawanyanyapaa na kuwadhalilisha. Ninataja ‘*kuelimika*’ kwa kuwa hoja hii iliibuliwa na wanavyuo walemaru pamoja na walemaru wasomi ambaa ni wanaharakati kama vile Kaganzi Rutachwamagyo ambaye aliwahi

kuwa mkurugenzi wa *Information Centre on Disability* (ICD) na wengineo. Hoja yao kuu kuhusu udhalilishaji wa majina hayo ilikuwa ni matumizi ya ngeli ya kitu au vitu (KI/VI) badala ya ngeli ya viumbe hai (M/WA).

Katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mnamo mwaka 2002-2006 kulikuwa na wanafunzi wenyewe ulemavu wapatao wanne ambao nilisoma nao shahada ya ualimu na somo la kufundishia likiwa ni Kiswahili. Wanafunzi hawa ndio walionifanya nianze kufanya utafiti ili kuona kwa nini ‘wanakataa’ kuitwa hivyo tulivyoza kuwaita. Hebu tujiulize, kuna tofauti gani kati ya ngeli ya KI/VI na M/WA? Ngeli ya KI/VI inahusisha vitu visivyo na uhai ambavyo huanza na kiambishi ‘ki’ katika umoja na ‘vi’ katika wingi. Nomino kama vile kiti-viti, kisu-visu, kioo-vioo na kiatu-viatu zinaingia katika ngeli hii. Kwa hiyo, kumwita mtu kilema-vilema, kipofu-vipofu na kiwete-viwete ni kumdhalilisha na kumfanya ajisikie vibaya kutokana na kulinganishwa na kitu. Kuhusiana na jina kiwete, mmoja wa watafitiwa wetu anaeleza kuwa “jina hili ni la kudhalilisha hata wewe mwenyewe ukifikiria kwenye akili yako...sawa hata kama unaonekana vile lakini ukiangalia kwa undani ni kama linakudhalilisha lile jina [...] hivi sasa sisi tumezoea kuita mlemau wa viungo”.

Kwa upande wa jina kipofu, walemaru waliohojiwa na mtafiti wanaeleza kuwa “jina hili linadhalilisha. Pia watu wazima huwa wana kejeli zao. Mtu anaweza kukukebehi tu na kusema: ‘kwani wewe kipofu’. Kwa hiyo unafanya rejea ya mtu mwagine kwa mambo mabaya.. Jina sahihi ambalo halidhalilishi ni asiyeona”. Hali hii ya kupinga kuitwa majina haya imejitokeza pia kwa jina zeruzeru. Utafiti wetu umebaini kuwa “jina hili katika baadhi ya tamaduni za Kiafrika linamaanisha ‘mtoto wa shetani’. Hivyo, watu wengine hudhani moja kwa moja kuwa zeruzeru ni ‘mtoto wa shetani’...Jamii haina budi kuachana na jina zeruzeru na badala yake kutumia jina albino”.

Kwa mujibu wa mazungumzo na walemaru hao, wanapendekeza ngeli ya viumbe hai ndiyo itumike kuwarejelea. Ngeli hii ya M/WA inahusisha viumbe hai ambao ni pamoja na wanyama, wadudu, ndege, na kadhalika. Binadamu ni kiumbe hai, ni mnyama, kwa hiyo jina linalomtambulisha mtu linapatikana katika ngeli hii ukiachilia mbali nomino zinazoanza na ‘ki/vi’ kama vile kijana/vijana; kiongozi/viongozi; na kingunge/vingunge kwani majina haya hayaashirii dosari za kimwili. Kuna majina kama vile mtu-watu, mtoto-watoto, mzee-wazee, mjomba-wajomba, na kadhalika. Ngeli hii ndiyo inayotambulisha watu kwa hiyo walemaru nao ni watu. Kwa mantiki hiyo, majina yanayorejelea ulemavu yanatakiwa yatokane na ngeli hii. Ndiyo maana tuna majina na vitenzi mbadala kama vile mlemau/walemaru; asiyeona/wasioona; mwenye umbile fupi/wenye maumbile mafupi, na kadhalika.

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977), haki za binadamu ni pamoja na: haki ya usawa, kuishi, kupata elimu, kujumuika, kwenda kokote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kushiriki katika jamii, kupata taarifa, usawa wa kutambuliwa kama mtu mbele ya sheria, kuheshimiwa, kutokubaguliwa, uhuru wa kujieleza, uhuru wa kutoa mawazo, ajira, kuwa na familia, kupiga kura, na uhuru wa kuabudu dini unayoipenda. Sababu ya makala haya kuihusisha Katiba ya nchi yetu ni kutaka kupata msingi wa kisheria kuhusu haki ya kuheshimiwa ambayo walemovu wanaona inakiukwa. Majina wanayoitwa walemovu nchini Tanzania yanakiuka haki ya 'kuheshimiwa'. Jambo hili ni kinyume cha sheria na Katiba ya nchi. Katiba inamtaka kila mtu aheshimiwe utu wake kwa kuwa watu wote wako sawa mbele ya sheria. Je, ni kweli walemovu 'wanavunjiwa' heshima na watumiaji wa lugha ya Kiswahili?

Madai haya ya kutoheshimiwa yanathibitishwa pia na kitabu kinachoitwa *Maadili kuhusu Ulemavu* kilichoandikwa na ICD na kuchapishwa mwaka 2002 kwa msaada wa Ubalozi wa Ufini nchini Tanzania. Kitabu hiki kinaonesha majina yenye kejeli ambayo wanaitwa watu wenye ulemavu na ambayo yanawadhalilisha. Mwandishi wa kitabu hiki anasema hivi:

"Majina yenye kejeli ni udhalilishaji wa utu wa mhusika hivyo kuwa chanzo cha kumtenga na kumsababishia sononi. Mpe haki ya kuchagua jinsi anavyotaka aitwe (ICD, 2002:1)".

Nukuu hii inaelezea majina wanayoitwa walemovu ambayo ni: 'kipofu', 'zeruzeru', 'kiziwi', 'kichaa', 'zezeta', 'taahira', 'mbilikimo', 'kilema', 'kiwete', na 'asiyejiweza' kuwa yanawakejeli na kuwafanya wajisikie kudhalilishwa utu wao. Majina hayo yanamfanya mlemapu ajisikie kutengwa na jamii yake na kumsababishia sononeko moyoni. Kwa hiyo, inashauriwa kuwa watu wasio na ulemavu wakubali mabadiliko. Wakubali kuwaita walemovu majina mazuri ambayo walemovu wanayataka. Mathalani, Kamusi ya Kiswahili Sanifu (TUKI, 2000) inafasili baadhi ya majina hayo ya walemovu kama ifuatavyo:

- Kilema: i. "ni kasoro iliyoko kwenye kiungo au viungo vyatya mwili"; "uatilifu".
ii. "mtu mwenye upungufu wa kiungo kama vile kiwete" (TUKI, 2000: 169).
- Kiwete: "ni mtu aliyelemaa miguu yote miwili" (TUKI, 2000: 187).
- Kipofu: "ni mtu asiyeona kutokana na kuugua, ajali, au kuzaliwa hivyo" (TUKI, 2000:176).
- Zeruzeru: "ni mtu ambaye nywele na ngozi yake imekosa rangi yake kamili na badala yake kuwa nyeupe sana na ambaye macho yake hayawezi

kuvumilia mwangaza mwingi," "albino" (TUKI, 2000: 467).

Hizo ndizo maana za majina hayo yanavyoelezwa kwenye kamusi. Maana hizo au majina hayo ndiyo yanayoibusha msigano. Ni msigano kwa kuwa, wanajamii ambaao ni wazungumzaji wa Kiswahili, ambaao sio walemaru, wanayatumia majina hayo kuwarejelea watu wenye ulemavu. Na kwa upande mwingine, walemaru wanayakataa majina hayo na kudai kuwa yanawadhalilisha. Badala yake, walemaru wana fasili yao kuhusu ulemavu na vilevile wana majina yao mbadala ambayo wanataka warejelewe kwayo, kama inavyopendekezwa hapa chini:

7.0 Watu wenye Ulemavu Wanapendekeza Waitweje?

Pendekezo la kubadilisha majina hayo yenyewe dharau na kebehi linatolewa katika kitabu cha *Maadili kuhusu Walemaru* (ICD, 2002:1) na pia watafitiwa wa utafiti wetu. Majina hayo ndiyo wanayoyapendekeza walemaru wa Tanzania kuitia Kituo cha Habari Kuhusu Ulemavu. Majina hayo ni: 'asiyeona', 'albino', 'kiziwi', 'mwenye ugonjwa wa akili', 'mwenye ulemavu wa akili', 'mwenye umbile fupi', 'mlema', 'mlema wa viungo', na 'mtu mwenye ulemavu' (ICD, 2002:1). Tutazame orodha ya majina hapa chini ambapo katika upande wa kushoto, kuna majina ambayo walemaru hawayapendi na upande wa kulia kuna majina ambayo walemaru wanapenda warejelewe:

Badala ya Kuita...	Ita Hivi...
Kipofu.....	asiyeona
Zeruzeru, mlema wa ngozi.....	albino
Asiyesikia.....	kiziwi
Kichaa.....	mwenye ugonjwa wa akili
Zezeta, taahira.....	mwenye ulemavu wa akili
Kifafa.....	mwenye kifafa
Mbilikimo.....	mwenye umbile fupi
Kilema.....	mlema
Kiwete.....	mlema wa viungo
Asiyejiweza.....	mtu mwenye ulemavu

Katika orodha hiyo, neno 'asiyejiweza' halimaanishi maskini bali wanaolitumia wanamaanisha mtu ambaye ana ulemavu, yaani anayehitaji msaada fulani ili aweze kutenda jambo fulani. Mathalani, mlema wa miguu ambaye hawezi kutembea huenda anahitaji kubebwa kama njia ya kujongea; ama la anatumia kitimwendo au baiskeli ya magurudumu kwa hiyo anahitaji kusukumwa. Umaskini sio ulemavu.

8.0 Hitimisho

Makala yameona kuwa maana ya ulemavu inatofautiana kimtazamo baina ya watu wenye ulemavu na wale wasio na ulemavu. Utafiti umebaini na kuthibitisha kuwa kuna msigano wa majina waitwayo wale mavu katika jamii ya wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili nchini Tanzania. Hakuna budi wadau husika wa mambo ya lugha wakiwemo wataalamu wa Kiswahili na watunzi wa kamusi, kukaa pamoja na watu wenye ulemavu mbalimbali ili kuzungumza na kuafikiana namna wanavyotaka kutambuliwa katika jamii. Ikifikia hatua hiyo, tupate Kamusi ya Kiswahili Sanifu ambayo imezingatia mahitaji maalumu ya watu wenye ulemavu. Kamusi ambayo ni jumuishi na itakayowafanya wazungumzaji wote wa Kiswahili wajisikie vizuri kuhusiana na lugha yao.

Halikadhalika, jamii haina budi kubadili namna ya kuwaita wale mavu hao. Vilevile, kwa kuzingatia haki za binadamu hasa kipengele cha kuheshimiwa, wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili hawana budi ku waheshimu wale mavu kwa kuwa ni haki ya msingi ya kila raia wa Tanzania kuheshimiwa. Lugha ya kebehi, dharau na inayolenga dosari za kimaumbile za watu wenye ulemavu iepukwe kwa nguvu zote. Nikisema hivi ninamaanisha kuwa, watu wenye ulemavu wana majina yao waliyopewa na wazazi wao, tusiwape majina kwa kurejelea hitilafu za miili yao. Mathalani, kama mtu ambaye si mlemau lakini ana dosari ya kukojoa kitandani akiwa usingizini, atajisikiaje akiitwa ‘kikojozi’ mbele ya wanajamii, watoto wake, au watu wake anaowaheshimu? Bila shaka mtu huyu atajisikia vibaya na huenda akaonyesha mrejesho hasi kutokana na kuitwa hivyo. Wito wa makala haya ni kuhimiza mabadiliko katika jamii hususan matumizi ya lugha inayotumika kuwarejelea watu wenye ulemavu.

Marejeo

- Besha, M. R. (2007). *Utangulizi wa Lugha na Isimu*. Dar es Salaam: Macmillan Aidan Limited.
- CCBRT, (2010), *Persons With Disability Act*. Dar es Salaam: Mpiga Chapa wa Serikali.
- ICD, (2002). *Maadili kuhusu Ulemavu*. Dar es Salaam: Ubalozi wa Ufini Tanzania.
- ILO, (2007). *Kufanikisha Fursa Sawa za Ajira kwa Watu wenye Ulemavu kupitia Sheria: Mwongozo*, Dar es Salaam.
- Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wizara ya Ajira, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Sera ya Taifa Kuhusu Ulemavu. Mpiga Chapa wa Serikali : Dar es Salaam.
- Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa

- Umma, (h.t.), *Mwongozo Kuhusu Watumishi Wenye Ulemavu*. Mpiga Chapa wa Serikali : Dar es Salaam.
- Mahenge, E. (2010). "Baadhi ya Changamoto Zinazowakibili Walemovu wa Tanzania", (haijachapishwa. Iliwasilishwa kwenye Tamasha la Sauti za Kiswahili lililoandaliwa na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Mwaka 2010 katika Hoteli ya Elephant – Dar es salaam).
- Mahenge, E. (2011) *Walemovu wa Tanzania*. Carolina: North Carolina Co Ltd.
- Muzale, H. T. R. (2004). *Kamusi ya Lughya ya Alama ya Tanzania (LAT)*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mwakyusa, D. (2008). *Jamhuri ya Muungano wa Tanzania: Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii*, Taarifa ya Mheshimiwa Profesa David Homeli Mwakyusa (MB), Waziri wa Afya na Ustawi wa jamii kwa vyombo vya habari kuhusu matokeo ya awali ya utafiti uliofanyika mwaka 2008 juu ya watu wenyewe ulemavu Tanzania.
- Massamba, D.P.B, Kihore, Y.M, Hokororo, J.I. (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA)*. Dar es Salaam: TUKI.
- United Republic of Tanzania (URT): Ministry of Labour, Youth Development and Sports. (2004). *National Policy on Disability*, Dar es Salaam.
- United Republic of Tanzania. (1977). *The Constitution of United Republic of Tanzania*. Dar es Salaam.
- United Republic of Tanzania. (2010). *Persons With Disability Act*. www.ccbrt.or.tz/.../Summary of Persons with Disabilities Act 201.
- Rutachwamagyo, K. (2000). *Dhana ya Elimu Jumuishi: Ulemavu na Haki ya Elimu nchini Tanzania*. Dar es Salaam.
- TUKI (2000) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.

Baadhi ya Mahojiano kati ya Mtafiti na Watu wenyе Ulemavu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

- Swali: Ninapenda kufahamu maana ya mlemavu kwa mtazamo wako.
- Jibu: Mtu mwenye ulemavu ni binadamu yeote wa kawaida kama ulivyo wewe au kama mtu mwingine ambaye wewe unamfahamu. Lakini mpaka aitwe mwenye ulemavu ana kasoro zinazomfanya aonekane yuko tofauti na mwenzake kimtazamo, kimwili au kiakili na vinginevyo ambavyo tutazungumza huko mbele.
- Swali: Ulemavu ni nini?
- Jibu: Ni ile hali ya mtu kutomudu kufanya kitu kwa uwezo wake yeye mwenyewe. Mathalani, mtu amekatika mikono miwili hawezi kulima – huyu ni mwenye ulemavu. Kule kukatika mikono yake ndicho kilema chake ... kwa hiyo, kile kikwazo chake mimi naweza kukiita kilema chake. Lakini kuna baadhi ya watu wamekuwa wakiwaita watu ‘kilema’. Mimi binafsi siwezi kumwita mtu kilema ila nitamwita mlemavu. Kilema ni ile hali inayomfanya aonekane vile kuwa na mapungufu fulani: kile ndicho kilema chake.
- Swali: Nimesikia kuwa baadhi ya majina wanayoitwa watu wenyе ulemavu, wenyewe hawayapendi, majina kama **kilema**, **kiwete**, **zeruzeru**, **kipofu**, **kiziwi**. Wewe unasemaje?
- Jibu: Haya majina ya watu wenyе ulemavu mzizi wake ni wa kizamani. Baadhi ya majina haya mzizi wake unatokana na mila na desturi kutoka maeneo mbalimbali ya Watanzania na Waafrika pengine hata Wazungu. Mkifanya utafiti mtabaini labda walivyokuwa wanawaita watu wenyе ulemavu [...] Kwa hiyo naweza nikakubali baadhi ya majina hayo lakini kuna mengine naweza nikatoa hoja...Kwa mfano neno ‘**kiziwi**’. Sina tatizo na neno kiziwi lakini nina tatizo na mtu anayeendelea kusema kwamba yule mtu ‘**hasikii**’. Kwa sababu mtu asiyesikia katika jadi yetu ni mkaidi, mwenye kiburi, maringo, majivuno, juha [...]
- Swali: Vipi kuhusu jina **kiwete**?
- Jibu: Jina hili ni la kudhalilisha, hata wewe mwenyewe ukifikiria kwenye akili yako ... sawa, hata kama unaonekana vile, lakini ukiangalia kwa undani ni kama linakudhalilisha lile jina [...] hivi sasa sisi tumezoea kuita **mlemavu wa viungo** [...]
- Swali: Kuna tofauti gani kati ya **zeruzeru** na **albino**?
- Jibu: Jina hili ‘**albino**’ lina asili ya nchi za Kigiriki. Neno ambalo linamaanisha kwenye tamaduni zao `nyeupe au yenye rangi nyeupe’. Albino ni binadamu aliyekosa seli za kutengeneza rangi katika mwili wake kutokana na sababu za kibiolojia. Hapa Tanzania tulikuwa tunaita ‘**zeruzeru**’. Lakini wanaharakati walikaa wakatafakari na

kuona jina hili linatumika kama kejeli. Jina hili katika baadhi ya tamaduni zetu linamaanisha ‘**mtoto wa shetani**’. Jina hili la ‘zeruzeru’ linadhalilisha na watu wengine wanakwenda moja kwa moja na kusema kuwa zeruzeru ni ‘mtoto wa shetani’. Kwa hiyo, mtu mwenye ulemavu akapewa upendo na jamii inashawishiwa ikubali kuachana na jina ‘zeruzeru’[...]

Swali: Jina **kipofu** nalo unalizungumziaje?

Jibu: Jina hili linadhalilisha. Na pia watu wazima huwa wana kejeli zao. Mtu anaweza kukukebehi tu na kusema: ‘kwani wewe kipofu’. Kwa hiyo unafanya rejea mtu mwengine kwa mambo mabaya [...]. Jina sahihi ambalo halidhalilishi ni ‘**asiyeona**’.

